SHULE YA SEKONDARI MASUGURU

S.L.P 246

NANYUMBU

18/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI

……..………………………………………………..……………………………….

S.L.P 246

NANYUMBU.

YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASUGURU WILAYA YA NANYUMBU MKOA WA MTWARA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tatehe 11/01/2021 na mwisho tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba (7)

2.0 MAMBO YA KUZINGATIA

2.1 sare za shule

a) Sare za shule hii ni kama ifuatavyo

1. Kwa wavulana
   - Suruali yenye linda rangi ya zambarau kitambaa cha suti chenye ubora upana wa chini ( turn up) isipungue saizi 18. Ziwe mbili (2)
   - Shati jeupe la mikono mifupi. Yawe mawili (2)
   - Viatu vyeusi vya ngozi pea mbili
   - Soksi nyeupe pea mbili
2. Kwa wasichana
   - Sketi rangi ya zambarau mshono rinda box urefu izidi magoti na kitambaa cha suti chenye ubora. Ziwe bili(2)
   - Shati jeupe mikono mifupi. Yawe mawili (2) au
   - Nusukanzu rangi nyeupe. Ziwe mbili (2)
   - Kwa watakaovaa hijabu rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule
3. Sare za michezo kwa wavulana
   - Jezi ya blue na raba
4. Sare ya michezo kwa wasichana
   - Trakisuti ya bluu na raba

3.0 VIFAA VINGINE MUHIMU VYA VYA MWANAFUNZI

1. Counter book Q2 kumi (10)
2. Daftari kubwa za mazoezi kumi (10)
3. Kalamu na mkebe wa hesabu
4. Kamusi (Dictionary) Oxford

5. Bima ya afya
6. Rim paper 1

4.0 VIFAA VYA USAFI

- Ndoo ndogo moja (1)
- Fagio la chelewa ( makuti)
- Jembe au kwanja

5.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Shule hii inaendeshwa na sheria pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya raisi TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
h) Kutunza mali za umma

6.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Usharati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya uma
g) Kudharau bendera ya taifa
h) Kuoa au kuolewa
i) Kutoa mimba
j) Kugoma, kuchochea na kuongozana au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu ya mkononi.

7.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI;

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitari ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mala utakaporipoti shuleni.
b) Vifaa vyote vilivyoagizwa MWANAFUNZI anapaswa aje navyo shuleni siku ya kuripoti ili vikaguliwe

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA

JINA LA MKUU WA SHULE ………………………………………………………… SAHIHI……………………………………